# Usafiri Ardhini

ISSN 2961 - 6255

JANUARI - MACHI, 2026

Toleo la 10



# KAMATI YA PIC YAITAKA LATRA KUWADHIBITI WANAOCHEZEA VTD

Uk 13



**CPA, DKT. HABIBU SULUO**
**MKURUGENZI MKUU - LATRA**

# TAHARIRI

Sekta ya usafiri ardhini inaendelea kuwa mhimili muhimu wa ukuaji wa uchumi, utoaji wa huduma za kijamii pamoja na kuunganisha watu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Kutokana na umuhimu huo, juhudi za kuendelea kuboresha mifumo ya usafiri salama, wa uhakika na unaozingatia mahitaji ya wananchi zimeendelea kupewa kipaumbele na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya Usafiri Ardhini nchini.

Jarida hili limebeba simulizi za mafanikio, mafunzo, maboresho ya huduma na ushiriki wa wadau katika kujenga sekta ya usafiri inayokidhi matarajio ya wananchi yanayoakisi Dira ya maendeleo ya taifa 2050. Juhudi hizi zimeendelea kutekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026.

Miongoni mwa habari zilizopo katika jarida hili ni pamoja na agizo lililotolewa Februari 4, 2026 na Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi kwa LATRA, kuongeza kasi ya uthibitishaji wa madereva na usajili wa wahudumu wa mabasi ya mijini nchini. Hatua hiyo inalenga kuboresha huduma za usafiri wa umma, hususan kwa wanafunzi ili waweze kupata huduma za usafiri katika mazingira salama, rafiki na yenye staha.

Vilevile, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na LATRA imeendelea kushirikisha wadau katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya usafiri, ikiwemo kupokea maoni yanayochangia kuboresha sera, Sheria na Kanuni mbalimbali. Machi 17, 2026, Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa Njia ya Barabara Wizara ya Uchukuzi, aliongoza mkutano wa kutoa elimu na kupokea maoni kutoka kwa viongozi wa vyama vya madereva, vyama vya wamiliki wa malori na kampuni za usafirishaji wa mizigo kuhusu Rasimu ya Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu wa Madereva za mwaka 2026.

Aidha, Mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi muhimu wa usalama katika uendeshaji wa reli (Safety Critical Workers), wakiwemo madereva na waongoza treni za reli ya kisasa (SGR), kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi na kupunguza ajali zinazoweza kusababishwa na makosa ya kibinadamu.

Nikukaribishe sasa usome yaliyojiri katika jarida hili, naamini utahabarika na kujifunza. Mamlaka itaendelea kusimamia sekta inazozidhibiti kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha wadau wote wa usafiri ardhini wananufaika na sekta yao. Kwa maoni yoyote, usisite kuwasiliana nasi kwa namba zetu bila malipo 0800110019 / 0800110020 au kupitia Mfumo wa e-Mrejesho unaopatikana kwa anwani emrejesho.gov.go.tz au kwa kufika ofisi ya LATRA iliyo karibu yako. Pia, tutumie ushahidi wa video na picha zinazohusu uvunjifu wa Sheria za Usafiri Ardhini kwa namba ya WhatsApp 0681300800, nasi tutazifanyia kazi kwa wakati.

Nikutakie usomaji mwema wa jarida hili

***"Pamoja kwa Usafiri Bora"***

# KAMATI YA PIC YAITAKA LATRA KUWADHIBITI WANAOCHEZEA VTD

Mhe. Mha. Johnston Mutasingwa (Mb), Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu (PIC) ameitaka LATRA kuwadhibiti na kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaochezea Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD) kinachotuma taarifa kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kwa kuwa wanahatarisha maisha ya wananchi wanaotumia usafiri wa umma.

Mhe. Mutasingwa amebainisha hayo Februari 16, 2026 wakati wajumbe wa Kamati ya PIC walipotembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya ziara maalum ya kujifunza jinsi LATRA inavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

"Tumesikitika kuona bado wapo baadhi ya watu wanaochezea mfumo wa VTS, hivyo tumeielekeza LATRA kuwafuatilia na kuwadhibiti kwa kuwa wanawaweka hatiani watu wasio na hatia. Pia tumewasihi kufanya kazi kwa uweledi, uzalendo na kutimiza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuwa LATRA ina jukumu kubwa la kulinda uhai wa wananchi wanaotumia usafiri wa umma na kufuatilia vyombo vya moto wanavyovidhibiti," amesema Mhe. Mutasingwa.

Aidha, Kamati hiyo imeipongeza LATRA kwa kazi nzuri ya kuimarisha mifumo ya udhibiti ambayo imesaidia kupunguza ajali, "Tunaipongeza Serikali kupitia LATRA kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya udhibiti ajali kwa njia ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

*Inaendelea Uk 2 >>>*



*Mhe. Mha. Johnston Mutasingwa (Mb), Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu (PIC) akiongoza kikao cha pamoja na Menejimenti ya LATRA walipotembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza kuhusu kazi na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka, Februari 16, 2026.*

# KAMATI YA PIC YAITAKA LATRA KUWADHIBITI WANAOCHEZEA VTD

<<< *Inatoka Uk 1*

Tumejionea kazi kubwa inayofanywa hasa uimarishaji wa mifumo ya udhibiti mwendokasi, ambayo ni muhimu sana katika kuimarisha usalama."

Katika hatua nyingine, Kamati ya PIC imeiagiza LATRA kushirikiana na vyombo vyingine vya udhibiti na usalama barabarani ili kuhakikisha usafiri ardhini unakuwa bora na salama huku wadau wakitekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

Naye CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA ameieleza Kamati hiyo kuwa, LATRA imekuwa ikiwafikia wadau wake na kushirikiana nao katika masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya usafiri ardhini na wataendelea kushirikiana nao ili kuwa na sekta bora inayoendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na inayokidhi matakwa ya Serikali, wananchi na wasafirishaji kwa jumla.

Ziara hiyo ya siku moja imetoa fursa kwa wajumbe wa Kamati ya PIC kujionea jinsi LATRA inavyotumia mifumo ya TEHAMA kuhudumia wadau wake na pia walishuhudia moja kwa moja utahini wa madereva wa vyombo vya moto kibiashara unavyofanyika, hatua inayolenga kuhakikisha madereva wanazingatia Sheria Kanuni na Taratibu za usalama barabarani. Ziara hiyo ilitoa nafasi ya kubadilishana uzoefu na kuimarisha ushirikiano kati ya Kamati na LATRA katika kuendeleza sekta ya usafiri nchini.

---

# HUDUMA MAALUM YA BRT YARAHISISHA USAFIRI KWA WANAFUNZI

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA imeendelea kuboresha huduma za usafiri nchini ambapo kupitia mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) inatoa mabasi maalum kwa wanafunzi yanayowawezesha kufika shuleni kwa wakati.

Hayo yamebainishwa na Bw. Gabriel Katanga, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Masoko na Uhusiano kwa Umma UDART Machi 18, 2026 ambapo amesema Kampuni hiyo inatoa huduma maalum ya kubeba wanafunzi jijini Dar es Salaam kupitia awamu ya kwanza ya mradi wa BRT unaojumuisha barabara za Morogoro kutoka Kimara hadi Kivukoni, Kimara Gerezani na Kimara Morocco.

Vilevile amesema kuwa, huduma hiyo maalum imeanzishwa kwa dhumuni la kutatua changamoto ambazo wanafunzi wamekuwa wakikabiliana nazo katika usafiri wa mabasi ya mjini (daladala) kila siku nyakati za asubuhi wakienda shule na jioni wakirejea nyumbani.

Bw. Katanga amesema huduma hiyo maalum ina jumla ya mabasi manne, mabasi mawili hutolewa kila siku asubuhi saa 12 kutoka Kimara hadi Kivukoni na Kivukoni hadi Kimara, na mengine mawili hutolewa nyakati za jioni kuanzia saa 11.

"Kwetu sisi usalama wa wanafunzi ndio kipaumbele chetu kikuu, tunahakikisha wasimamizi wapo katika mabasi hayo na vituoni kuwasimamia wanafunzi wakiwa

*Inaendelea Uk 3* >>>

# HUDUMA MAALUM YA BRT YARAHISISHA USAFIRI KWA WANAFUNZI

*<<< Inatoka Uk 4*

ndani ya mabasi na wanapofika kwenye vituo vya mwisho," amesema Bw. Katanga.

Kwa upande wake Bw. Jumanne Omary, Msimamizi wa Kituo cha Kimara amesema kuwa, wameweka utaratibu maalum ambapo mabasi yanapangwa kwenye ratiba maalum unaowawezesha wanafunzi kupanda magari kwa utulivu na kushuka kwa utulivu.

Naye Mwanafunzi Jacqueline Peter ameipongeza Serikali kwa jitihada za kuboresha huduma ya usafiri kwa wanafunzi kupitia huduma ya BRT inayowawezesha wao kufika shuleni na kurudi nyumbani bila kuchelewa. "Kuna utofauti kati ya daladala na mabasi ya BRT kwakuwa yamerahisisha maisha yetu na kulinda wanafunzi dhidi ya usafiri wa kiholela. Tunaipongeza Serikali kwa uwepo wa miundombinu bora na kuelekeza nauli ya shilingi 200 kwa wanafunzi iliyowezesha huduma hii kuwa nafuu."

Kwa upande wake Bw. Godfrey Philimon mzazi wa mwanafunzi anayetumia huduma ya usafiri huo amefurahia uwepo wa huduma hiyo ambayo imewapa unafuu wazazi kuwalipia nauli ya mabasi hayo na imewapa uhakika watoto wao kufika shuleni salama na kwa wakati.

"Hali ya sasa ni tofauti na hapo awali, wanafunzi walikuwa wanajazana sana kituoni hali inayosababisha kuchelewa shuleni, lakini sasa ikifika saa 12 hadi saa moja asubuhi hukuti mwanafunzi yeyote kituoni kutokana na uhakika wa huduma ya usafiri huu, tunamshukuru sana Rais wetu kwa jitihada alizozifanya, nauli iliyoelekezwa na LATRA imetupa unafuu sisi wazazi hasa wenye hali ya chini kumudu gharama hizo," amesema Bw. Philimon.

Huduma hii ya BRT kwa wanafunzi ni mfano wa jitihada zinazotekelezwa na LATRA kwa kushirikiana na wadau kuhakikisha huduma za usafiri kwa wanafunzi jijini Dar es Salaam ni salama, za uhakika na zenye gharama nafuu.

> **"Kwetu sisi usalama wa wanafunzi ndio kipaumbele chetu kikuu. Tunahakikisha wasimamizi wapo katika mabasi hayo na vituoni kuwasimamia wanafunzi wakiwa ndani ya mabasi na wanapofika kwenye vituo vya mwisho"**
>
> ***Bw. Gabriel Katanga***



# ABIRIA WAASWA KUHAKIKI TIKETI ZAO KABLA YA KUANZA SAFARI




*CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, akikagua taarifa zilizopo kwenye tiketi ya kielektroni wakati wa ukaguzi wa mwisho wa mwaka, Desemba 23, 2025 Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli, Dar es Salaam.*

CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amewaasa abiria wanaosafiri kwa mabasi yaendayo mikoani kuhakiki tiketi zao za safari kupitia Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) unaojulikana kwa jina la Safari Tiketi unaopatikana kwa anwani ya tiketi.latra.go.tz ili kuepuka ulanguzi wa tiketi unaosababisha kutozwa nauli isiyokuwa elekezi.

CPA, Dkt. Suluo amebainisha hayo Desemba 23, 2025 wakati akifanya kaguzi za usafiri wa mabasi yaendayo mikoani katika vituo mbalimbali vya mabasi, kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka 2025.

"Tunawasisitiza abiria wote wanaosafiri hasa kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka na siku zote kuhakikisha taarifa zao za muhimu ikiwemo majina mawili au matatu yanakuwepo kwenye tiketi zao za safari kama ilivyo katika Kitambulisho Cha Taifa , hii itasaidia inapotokea dharura kujua nani alikuwa katika basi, kutokuwepo kwa taarifa hizo inasababisha ulanguzi wa tiketi," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Ameongeza kuwa, Mfumo wa Safari Tiketi unawezesha kumtambua abiria anayesafiri, kupata taarifa sahihi za abiria aliyekuwa safarini, kusuluhisha migogoro kwa abiria wawili waliokatiwa tiketi moja kwa kuhakiki tiketi kupitia mfumo na abiria anaweza kuhakiki tiketi yake mwenyewe.

Vilevile amesema, mbali na hali ya usafiri kuwa ni nzuri kutokana na abiria kusafiri bila msongamano, zipo baadhi ya changamoto zilizobainika katika vituo vya mabasi kwa baadhi ya wasafirishaji.

"Changamoto zilizobainika katika ukataji tiketi kwa baadhi ya abiria ni majina yao kutokuwepo kwenye Mfumo na wao kukabidhiwa tiketi ambazo zina jina tofauti, majina yao kuandikwa kwa kutumia kalamu ya mkono kwenye tiketi ileile yenye jina

*Inaendelea Uk 5 >>>*

## ABIRIA WAASWA KUHAKIKI TIKETI ZAO KABLA YA KUANZA SAFARI

*<<< Inatoka Uk 4*

jingine lakini ukihakiki tiketi hiyo kwenye Mfumo pia unakuta ina jina jingine hali inayosababisha tiketi moja kuwa na majina matatu tofauti," ameeleza CPA, Dkt. Suluo.

Wakati huohuo CPA, Dkt. Suluo ameeleza kuwa takwimu ya abiria waliosafiri Desemba 23, 2025 kuwa ni jumla ya abiria 120,279 na jumla ya abiria 2,198,076 wamesafiri katika kipindi chote cha sikukuu za mwisho wa mwaka na miamala yote ya jumla imefikia bilioni 79 na miamala iliyofanyika Desemba 23, 2025 ni billion 4 ambayo malipo yake yaliyofanyika mtandaoni uwiano ni uleule wa shilingi 449,000,000 sawa na asilimia 11.

Mfumo wa Safari Tiketi ni Mfumo uliounganishwa na mifumo mingine ya utoaji tiketi ukiwemo wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na mifumo ya tiketi za mabasi unaomwezesha abiria kufanya wekesho la safari kwa kampuni ya mabasi anayoitaka, kukata tiketi kimtandao na kufahamu basi analotaka kusafiri nalo liko sehemu gani kupitia Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS).

---

# ABIRIA WAASWA KUHAKIKI TIKETI ZAO KABLA YA KUANZA SAFARI

CPA, Dkt. Habibu Suluo Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema ushirikishwaji wa wadau ni nguzo muhimu katika kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini, hatua inayoongeza ufanisi, tija na kusaidia watoa huduma kutii sheria bila shuruti.

CPA, Dkt. Suluo amebainisha hayo Januari 19, 2026, katika kipindi cha dakika 45 kilichofanyika katika kituo cha habari cha ITV, ambapo ameeleza kuwa LATRA ina taratibu maalum za kuwashirikisha wadau wa sekta ya usafirishaji kabla ya kufanya mabadiliko yoyote katika utoaji wa huduma kwenye njia mbalimbali.

"Kabla ya kuwaondoa watoa huduma katika njia fulani au kuwasitishia leseni, hususan watoa huduma za usafiri wa daladala, ni lazima Mamlaka iwape mbinu mbadala na kuwaeleza mwelekeo wa mabadiliko yanayokusudiwa, mabadiliko ni mchakato unaohitaji maelewano na ushirikishwaji wa wadau ili kuhakikisha yanakubalika na kutekelezwa kwa ufanisi," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Aidha, CPA, Dkt. Suluo amesema LATRA tayari imefanya vikao na Umoja wa Wamiliki wa Daladala Dar es Salaam (DARCOBOA) pamoja na Umoja wa Wasafirishaji Abiria Dar es Salaam (UWADAR), ambapo wamejadili na kukubaliana namna ya kuwapa fursa ya kushiriki katika njia maalum, ikiwemo njia ya Gongolamboto, kwa mfumo wa uwekezaji unaozingatia maslahi ya wawekezaji wadogo.

LATRA inaendelea kuonesha dhamira ya dhati ya kushirikisha wadau, kurasimisha watoa huduma na kuboresha huduma za usafiri ardhini kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata usafiri salama, wa uhakika na wenye tija.

# WATOA HUDUMA WA MABASI YA MASAFA MAREFU WAPEWA SIKU 14 KUHAMIA KWENYE MIFUMO ILIYOIDHINISHWA NA LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewapa watoa huduma wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani siku 14 kuanzia tarehe 30 Januari, 2026 kuhamia kwenye mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa na Mamlaka. Hatua hiyo inalenga kuhakikisha utekelezaji kamili wa Kanuni za Tiketi Mtandao za mwaka 2024 na kuboresha udhibiti wa huduma za usafiri wa abiria nchini.

Akizungumza na waandishi wa Habari Januari 30, 2026, Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA amesema, mabasi yote yatakayokuwa bado yanatumia mifumo ya tiketi mtandao isiyoidhinishwa hayataruhusiwa kutoa huduma.

Vilevile amesema utoaji na uhuishaji wa leseni za usafirishaji wa abiria utazingatia matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa pekee.

"Hadi kufikia tarehe 30 Januari, 2026 jumla ya mifumo 10 ya tiketi mtandao imekidhi vigezo vya kisheria na kuidhinishwa kuendelea kutoa huduma, huku mifumo mingine ikizuiliwa kutokana na kushindwa kutimiza matakwa ya kisheria licha ya kupewa muda wa kutosha. Tunawasihi watoa huduma ambao bado hawajakamilisha taratibu za uidhinishaji kufanya hivyo ili waruhusiwe kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria," ameeleza Bw. Pazzy.

Aidha, Bw. Pazzy ameitaja mifumo iliyokidhi vigezo na kuidhinishwa kuwa ni AB Connect, Busbora, MySafari tiketi, Iyishe

*Inaendelea Uk 4 >>>*




*Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, akizungumza na vyombo vya habari kuhusu mifumo ya Tiketi Mtandao iliyoidhinishwa kutoa huduma kwa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani Januari 30, 2026 ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es salaam.*

# WATOA HUDUMA WA MABASI YA MASAFA MAREFU WAPEWA SIKU 14.....

<<< *Inatoka Uk 3*

Company Limited, Msafiri, Baspoa, Otapp, Afritech, Voltic Tanzania Limited na Web e-ticketing.

Ameongeza kuwa, ili mfumo upate kibali unapaswa uwe unamilikiwa na taasisi ya Serikali, chama cha ushirika au kampuni iliyosajiliwa Tanzania, uwe umeunganishwa na mfumo wa usimamizi wa malipo ya mapato wa kielektroni, uwe una uwezo wa kuunganishwa na mifumo ya Mamlaka, Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao, na mfumo wowote kama inavyohitajika, uwe umeidhinishwa na mamlaka zinazohusika, uwe wa kitanzania, uwe na mmiliki mwenye wafanyakazi wenye taaluma husika na uwe na ulinzi dhidi ya vamizi za kimtandao.

Kwa upande mwingine, LATRA imewakumbusha wasafirishaji kuhakikisha wanatumia wahudumu wa mabasi waliosajiliwa na Mamlaka hiyo na kuhakikisha kila abiria anasafiri akiwa na tiketi mtandao, abiria nao wametakiwa kununua tiketi kupitia mifumo iliyoidhinishwa na kutumia programu ya LATRA App kuhakiki tiketi na nauli halali, huku wakihimizwa kuwasilisha malalamiko yao kwa watoa huduma na kama hawajaridhika na suluhisho la msafirishaji wawasilishe LATRA kwa kupiga bila malipo kwa namba 0800110019 au 0800110020 au kupitia mfumo wa e-Mrejesho.

Hatua ya kuimarisha matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao inalenga kuwawezesha wasafirishaji kupata mapato kwa ufanisi bila kupitia watu wa kati, kuwasaidia abiria kununua tiketi kwa uwazi na urahisi, pamoja na kuzuia vitendo vya ulanguzi wa tiketi. Pia,matumizi ya mifumo hiyo yataisaidia Serikali kusimamia sekta ya usafiri kwa ufanisi zaidi na kuongeza uwazi katika ukusanyaji wa mapato.



# PROF. MBARAWA: ONGEZENI KASI YA UTHIBITISHAJI MADEREVA NA USAJILI WA WAHUDUMU WA MABASI YA MIJINI



*Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akizungumza na wanahabari (hawapo pichani) kuhusu hatua za serikali kuboresha usafiri wa wanafunzi katika maeneo ya mijini Februari 4, 2026 jijini Dodoma. Kulia ni CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA.*

Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi ameiagiza LATRA kuongeza kasi ya uthibitishaji madereva na usajili wa wahudumu wa mabasi ya mijini nchini ili kuboresha huduma za kijamii, hususan huduma za wanafunzi katika vyombo vya usafiri wa umma ili kuwawezesha kupata elimu katika mazingira rafiki na yenye staha.

Agizo hilo amelitoa Februari 4, 2026 jijini Dodoma alipozungumza na vyombo vya habari baada ya malalamiko yaliyotolewa na mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Mariana Eric Mirindima, aliyebainisha changamoto wanazokutana nazo wanafunzi wanapotumia usafiri wa mabasi ya mijini (daladala), ikiwa ni pamoja na kuchelewa kufika shuleni, kunyimwa huduma na usalama mdogo kutokana na baadhi ya watoa huduma kushindwa kuwahudumia wanafunzi kwa wakati unaofaa.

"Ninaiagiza LATRA kuhakikisha jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu (makondakta) kwenye mabasi linatekelezwa kwa kasi katika miji yote chini, na kutoa adhabu kali kwa mujibu wa Sheria kwa madereva na makondakta watakaobainika kuwanyanyasa wanafunzi na kuimarisha udhibiti wa nauli maalumu za wanafunzi, staha ya huduma na usalama wao kwa wakati wote," amesema Prof. Mbarawa.

Vilevile amesema, katika kukabiliana na changamoto za usafiri kwa wanafunzi mijini, Serikali imeweka mipango na

*Inaendelea Uk 6 >>>*

# PROF. MBARAWA: ONGEZENI KASI YA UTHIBITISHAJI MADEREVA...

<<< *Inatoka Uk 5*

mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sheria na Kanuni za kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya usafiri wa mabasi na treni, kuanzisha huduma za mabasi maalumu yaendayo haraka kwa ajili ya wanafunzi, kurasimisha na kusimamia utozaji wa nauli maalumu ya shilingi 200 kwa wanafunzi katika mabasi yaendayo haraka na daladala na kutenga mabehewa maalum kwa ajili ya wanafunzi kwenye treni za mijini jijini Dar es Salaam.

Pia, Prof. Mbarawa amesema LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wafanye ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushtukiza kwenye vituo vya daladala hasa nyakati za asubuhi na jioni kuhakikisha wanafunzi wanapata usafiri.

Ameongeza kuwa, Serikali inaendelea kusisitiza ushirikiano wa wadau wote ili kujenga mfumo wa usafiri wa umma unaolinda haki, usalama na ustawi wa wanafunzi na watu wote nchini na amewasihi Watanzania, na abiria kwa jumla, kushirikiana kuwatetea wanafunzi wanaponyanyaswa na mtu yeyote.

Mamlaka inaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi na wadau wote wa usafiri nchini kujenga mfumo wa usafiri wa umma unaolinda haki, usalama na ustawi wa wanafunzi na watu wote nchini. Pia, mwananchi anaweza kutuma ushahidi wa picha au sauti kwa vitendo vinavyokiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini kwa namba ya LATRA WhatsApp 0681 300 800

# SACCOS YA KWANZA KWA MAAFISA USAFIRISHAJI KUANZISHWA MKOANI NJOMBE

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Njombe imeanza utekelezaji wa mpango wa kuanzisha Chama cha Ushirika (SACCOS) cha kwanza cha maafisa usafirishaji wa Pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda) na magurudumu matatu (Bajaji) Mkoani Njombe hatua inayolenga kurasimisha shughuli za bodaboda na bajaji na kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi kupitia SACCOS.

Hayo yamebainishwa na Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Januari 6, 2026 wakati CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi mkuu LATRA alipofanya ziara mkoani Njombe kwa lengo la kukutana na kuzungumza na maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu.

Mhe. Mataka amesema kuwa, wazo la LATRA la kuanzisha SACCOS ni kubwa na linakwenda kutoa suluhisho la muda mrefu katika sekta ya usafirishaji Mkoa wa Njombe.

"Wazo hili litawezesha kazi ya Bodaboda na Bajaji kurasimishwa kama kazi nyingine kupitia SACCOS inayoenda kuanzishwa, wasafirishaji wataweza kujiwekea akiba zao, kuongeza kipato na kupata huduma za bima kama zilivyo ajira nyingine. Na Serikali ya Njombe ipo tayari kushirikiana na LATRA kuhakikisha SACCOS itakayoenda kuanzishwa inakuwa ya mfano wa kuigwa kitaifa na kuwa chombo muhimu cha kuwawezesha wasafirishaji kujikwamua kiuchumi," amesema Mhe. Mtaka".

Kwa upande wake CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema

*Inaendelea Uk 7* >>>

# SACCOS YA KWANZA KWA MAAFISA USAFIRISHAJI KUANZISHWA....

<<< *Inatoka Uk 6*

Mamlaka imeweka mkakati maalum wa kuwaangalia kwa karibu vijana wa sekta ya usafirishaji Mkoa wa Njombe kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri mkoani hapo.

"SACCOS hii inayoanzishwa Njombe itakuwa ya kwanza na ya mfano katika mkoa huu, mtazamo wetu ni kuwa na mfumo wa kidijiti utakaowaunganisha vijana wote wa usafirishaji kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya hadi Kata, utakaowawezesha kujitambua, kupata taarifa zao kwa urahisi na hatimaye kuunganishwa katika Mfumo wa Kitaifa, hatua itakayoboresha huduma za usafiri na kuongeza uwajibikaji kupata ushirikiano wa pamoja," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Ameongeza kuwa, Sheria ya LATRA imebaini umuhimu wa wasafirishaji wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu kujiendesha na kujisimamia wenyewe, hivyo kupendekeza uwepo wa vyama vya ushirika ambavyo baada ya kupitishwa kwa Kanuni husika, LATRA imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha uundaji wa SACCOS.

"Kabla ya kuwapatia uwakala wasafirishaji wanawasilisha maombi LATRA kupitia Mfumo wa Usimamizi na Utoaji Leseni za Usafiri wa Barabara na Reli (RRIMS) unaopatikana kwa anwani ya rrims.latra.go.tz na tukiridhika kuwa vigezo vimetimizwa, wanaanza kufanya kazi kupitia mfumo. Mapato yao yanaingia kwenye Mfumo wa LATRA kupitia namba ya malipo (control number) na kila mwezi tunawarejeshea asilimia 20 ya mapato wanayokusanya," amesema CPA, Dkt. Suluo.

*Inaendelea Uk 8* >>>



*Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe na CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi mkuu LATRA wakijadili jambo wakati Dkt. Suluo alipofanya ziara mkoani Njombe kwa lengo la kukutana na kuzungumza na maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu Januari 6, 2026*

# SACCOS YA KWANZA KWA MAAFISA USAFIRISHAJI KUANZISHWA....

*<<< Inatoka Uk 7*

Naye Dkt. Fredy Msemwa, Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango, amesema mpango wa kuanzishwa kwa SACCOS unaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, yenye lengo la kuchochea urasimishaji na kukuza sekta ndogo ya ushirika nchini.

"Kupitia SACCOS zitakazoanzishwa, vijana wa bodaboda wataweza kutambuliwa rasmi, kuweka malengo ya maendeleo na kupata fursa za kiuchumi ambazo mtu mmoja mmoja asingezifikia," amesema Dkt. Msemwa.

Vilevile amesema kuwa, Tume ya Taifa ya Mipango iko tayari kufanya kazi kwa karibu na LATRA kuhakikisha mpango wa uanzishwaji wa SACCOS unafanikiwa, hususan katika kuwaunganisha vijana katika mifumo ya akiba na kuwawezesha kujisimamia kiuchumi.

Kwa upande wake Bw. Vermud Msigwa, Mwenyekiti wa Maafisa Usafirishaji Mkoa wa Njombe, ameishukuru Serikali na LATRA kwa fursa ya mchakato wa kuanzisha SACCOS mkoa wa Njombe na kusema kuwa utawasaidia wasafirishaji kusaidiana wenyewe kwa wenyewe na kupata mikopo yenye riba nafuu isiyo na masharti kandamizi.

LATRA inaendelea kusisitiza ushirikiano wa wadau wote kuhakikisha sekta ya usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu inakuwa rasmi, salama, yenye tija na inayochangia maendeleo ya vijana na taifa kwa jumla.




*Bi. Nancy Amani, Afisa Uhusiano LATRA (kulia) na Bw. Herman Kinyariri Afisa Huduma kwa Wateja LATRA wakitoa elimu kwa wadau walipotembelea banda la LATRA katika Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar (ZITF) Kituo cha Maonesho Dimani, Fumba – Zanzibar Januari 6, 2026.*

# WANAFUNZI NA WAFANYABIASHARA WANUFAIKA NA HUDUMA ZA MOFAT




Wanafunzi na wafanyabiashara wa samaki jijini Dar es Salaam wameendelea kunufaika na huduma maalum za usafiri zinazotolewa na kampuni ya MOFAT katika mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) awamu ya pili ambapo huduma hiyo imewezesha wanafunzi kufika shuleni kwa wakati na kuongeza ufanisi kwa wafanyabiashara.

Bw. Ramadhan Ally, Afisa Masoko wa MOFAT amesema hayo Machi 10, 2026 na kubainisha kuwa, huduma hiyo imeanzishwa mahsusi ili kukabiliana na changamoto za usafiri kwa wanafunzi na wafanyabiashara wa samaki wanaosafiri kati ya Kivukoni na Mbagala, kwa kuhakikisha wanapata huduma za usafiri zilizo salama, za uhakika na kwa wakati.

"Tuliona ni muhimu kuanzisha huduma maalum kwa wanafunzi ili waweze kupanda mabasi yao wenyewe bila kuchanganyika na watu wazima, tunajivunia kufanikisha jambo hili na tunapata mrejesho mzuri kutoka kwa wazazi ambao wanakiri kuwa wameridhika na huduma hii kwa kuwa watoto wao wanafika shuleni kwa wakati bila usumbufu," ameeleza Bw. Ally.

Ameongeza kuwa, kwa sasa mabasi manne maalum yanawachukua wanafunzi kituoni kuanzia saa 11 alfajiri na kuwarudisha kuanzia saa 10 alasiri. Pia amesema, huduma hiyo imeanza takribani miezi sita iliyopita na inaendelea kuboreshwa kwa kuzingatia maoni ya wadau.

Wakati huo huo, Bw. Ally amesema MOFAT imepanua huduma zake kwa kuwafikia wafanyabiashara wadogo, hususan wa samaki, wanaosafiri kati ya Kivukoni, Mbagala na Ilala, ambapo huduma hiyo hutolewa kwa njia tano kila siku kuanzia asubuhi hadi jioni, na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zao kwa wakati.

*Inaendelea Uk 10* >>>

# WANAFUNZI NA WAFANYABIASHARA WANUFAIKA NA HUDUMA ZA MOFAT

<<< *Inatoka Uk 9*

Baadhi ya wanafunzi wanaotumia huduma hiyo wamesema awali walikuwa wakipoteza muda mwingi kusubiri mabasi, lakini tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo maalum, sasa wanafika shuleni kwa wakati na kurudi nyumbani mapema. Aidha, wamepongeza huduma inayotolewa ikiwemo kulipa nauli inayotakiwa yaani TZS. 200 na kurejeshewa chenji sahihi pindi wanapotoa fedha kubwa.

Kwa upande wake, Bw. Makongoro Timothy, dereva wa MOFAT amesema madereva wanazingatia taratibu zote za usalama barabarani na kutekeleza majukumu yao kwa umakini ili kuhakikisha abiria wanapata huduma bora.

Naye Bi. Salma Omary, mfanyabiashara wa samaki, amesema huduma hiyo imewarahisishia usafiri kwenda Kivukoni kununua samaki na kurejea kwa wakati hivyo kupunguza hasara iliyokuwa ikitokana na kuharibika kwa bidhaa kutokana na ucheleweshaji wa usafiri.

Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na LATRA inaendelea na jitihada za kuboresha usafiri ardhini nchini ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa kuzingatia Sheria zilizopo.

# MAGOMBANA: MAONI YA WADAU NI MUHIMU KUBORESHA KANUNI ZA UCHOVU WA MADEREVA

Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa Njia ya Barabara, Wizara ya Uchukuzi, amesema kuwa maoni ya wadau ni nyenzo muhimu katika kuboresha Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu wa Madereva za Mwaka 2026.

Amesema hayo alipomuwakilisha Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, katika mkutano wa kutoa elimu na kupokea maoni ya viongozi wa vyama vya madereva na viongozi wa vyama vya malori Tanzania na wamiliki wa kampuni za usafiri wa malori nchini kuhusu rasimu ya kanuni hizo Machi 17, 2026 ofisi za LATRA, Dar es Salaam,

Bw. Magombana amesema, kanuni hizo zinalenga kuhakikisha madereva wa vyombo vya moto kibiashara wanaendesha wakiwa na utimamu wa mwili na akili, hatua itakayochangia kupunguza ajali za barabarani na kulinda maisha ya abiria.

"Kanuni hizi zinalenga kuhakikisha madereva wanafanya kazi wakiwa na afya bora ya mwili na akili. Tukifanikiwa kudhibiti uendeshaji katika hali ya uchovu, tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani pamoja na usumbufu kwa abiria," amesema Bw. Magombana.

Aidha, amesisitiza kuwa ushirikishwaji wa wadau unaiwezesha Serikali kupata maoni yenye tija kutoka kwa wadau wanaofahamu hali halisi ya sekta ya usafiri, jambo linalochangia kuboresha sera na kanuni mbalimbali.

Kwa upande wake, Bi. Esnath Mwakyembe, Kaimu Meneja wa Uthibitishaji Madereva na Usajili wa Wahudumu, akimuwakilisha CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema

*Inaendelea Uk 14* >>>

# MAGOMBANA: MAONI YA WADAU NI MUHIMU KUBORESHA KANUNI ZA UCHOVU WA..

*<<< Inatoka Uk 13*

Mamlaka imewahimiza viongozi wa vyama vya madereva kuwashirikisha wanachama wao kikamilifu ili kutoa maoni kuhusu rasimu hiyo.

"Tumetoa elimu na kufungua fursa ya wadau kutoa maoni yao. Tunawasihi viongozi kuhakikisha wanawafikia madereva wote ili kushiriki kikamilifu katika uboreshaji wa kanuni hizi. Mamlaka itaendelea kupokea maoni kwa kipindi cha siku 14 kuanzia Machi 17, 2026," amesema Bi. Mwakyembe.

Naye Bw. Greyson Wimile, Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (CHAWAMATA), amesema chama hicho kimepokea rasimu za Kanuni hizo na kiko tayari kushirikisha wanachama wake pamoja na wataalamu wa Sheria ili kuwasilisha mapendekezo yatakayosaidia kuboresha Kanuni hizo ndani ya muda uliotolewa.

Kwa upande wake Bw. Michael Likingo, Meneja wa Mafunzo kwa Madereva kutoka kampuni ya Superstar, amesema ni muhimu kwa wamiliki wa malori kuweka mifumo madhubuti ya usalama, ikiwemo utoaji wa mafunzo endelevu kwa madereva pamoja na matumizi ya teknolojia za kufuatilia mienendo ya madereva wanapokuwa safarini kwani ni muhimu katika kutatua madhara yanayosababishwa na uchovu wa dereva.

Rasimu ya Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu wa Madereva inaweka msisitizo katika kuimarisha usalama barabarani kupitia udhibiti wa uchovu kwa madereva, hatua inayotarajiwa kupunguza ajali, kulinda maisha ya abiria na kuongeza ufanisi katika sekta ya usafiri ardhini.




*Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa njia ya Barabara, Wizara ya Uchukuzi akiongoza kikao cha kutoa elimu na kupokea maoni ya wadau kuhusu rasimu za Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu wa Madereva za Mwaka 2026. Kikao hicho kimefanyika ofisi za LATRA Dar es Salaam, Machi 17, 2026.*




*Baadhi ya Wanawake watumishi wa LATRA wakishiriki Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yaliyoadhimishwa Kimkoa katika Viwanja vya Barafu, Mburahati Dar es Salaam Machi 8, 2026 yenye Kaulimbiu "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana: Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050".*

*Wadau wa sekta ya usafiri ardhini wakipatiwa mafunzo kuhusu mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa na LATRA katika utekelezaji wa majukumu yake. Mafunzo hayo yamefanyika Machi 11, 2026 ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Dar es Salaam.*





*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu (PIC) pamoja na Menejimenti ya LATRA walipotembelea kituo cha kutahini madereva wakielezewa taratibu za kuthibibisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa, Februari 16, 2026, Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.*

# URASIMISHAJI WA MAAFISA USAFIRISHAJI WAIMARISHA NIDHAMU



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imebainisha kuwa, urasimishaji wa maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili (Bodaboda) na utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwa maafisa hao ni nguzo muhimu ya kuimarisha udhibiti wa vurugu na ukiukwaji wa Sheria unaofanywa na baadhi ya waendesha pikipiki barabarani.

Hayo yamebainishwa na Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, Februari 19, 2026 katika kipindi cha dakika 45, kituo cha habari ITV ambapo mada ilikuwa “Nini kifanyike kudhibiti vurugu za waendesha bodaboda barabarani kwa usalama wao na watumiaji wengine wa barabara.”

Bw. Pazzy ameeleza kuwa, Serikali kupitia LATRA imepiga hatua kubwa katika kurasimisha shughuli za bodaboda na kuwawezesha vijana kujikwamua kiuchumi kupitia SACCOS hali iliyoongeza usalama, nidhamu na ustawi wa waendesha pikipiki pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

“LATRA imewarasimisha waendesha bodaboda kwa kuwatambua kupitia vyama vya ushirika kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka, hatua inayowapa hadhi na heshima kama ajira nyingine rasmi. Kupitia urasimishaji huu, waendesha bodaboda wamewezeshwa kuwa mawakala wa utoaji wa leseni za LATRA na wanapata kamisheni ya asilimia 20 kama ambayo inawasaidia kujikwamua kiuchumi na kujisimamia wao wenyewe,” amesema Bw. Pazzy.

Ameongeza kuwa, kwa sasa LATRA ina mawakala zaidi ya 40 nchi nzima, na kwamba kwa mwezi wa Januari pekee jumla ya shilingi milioni 89 zililipwa kwa mawakala wa vyama vya usafirishaji ikiwa

*Inaendelea Uk 17 >>>*

# URASIMISHAJI WA MAAFISA USAFIRISHAJI WAIMARISHA NIDHAMU

<<< *Inatoka Uk 16*

ni kamisheni ya asilimia 20 ya makusanyo ya leseni za LATRA, hali inayochangia kuheshimika na kuwafanya wajisikie wenye thamani wanapokuwa barabarani.

Vilevile amesema, LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, inaendelea kuweka mifumo ya usajili itakayowawezesha waendesha bodaboda kupata leseni popote walipo, kuendelea kuwafikia na kuwapatia elimu ya usalama barabarani nchi nzima kupitia vyama vyao.

Kwa upande wake, SSP Solomon Mwangamilo, Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Kinondoni, amesema bodaboda ni chombo cha moto, hivyo ni lazima waendeshaji wake wazingatie Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Dereva wa bodaboda anatakiwa kuwa na leseni halali ya kuendesha chombo, bima, pamoja na kuhakikisha pikipiki ina ubora unaoruhusu kuendeshwa barabarani bila kuhatarisha maisha ya wengine.

Vilevile SSP Mwangamilo amesema, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kimeanzisha madawati ya elimu ya usalama barabarani kuanzia ngazi ya kata, wilaya hadi taifa, kwa lengo la kuwajengea uwezo waendesha bodaboda kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji salama.

"Tangu kuanza kutoa elimu, tumeshuhudia kupungua kwa ajali na vurugu. Zamani bodaboda walikuwa wakisababisha ajali na kuanzisha vurugu, lakini sasa uelewa umeongezeka. Pia Jeshi la Polisi linaendelea kufanya operesheni dhidi ya wavunjaji wa Sheria, na wale wanaokamatwa hupelekwa katika madawati ya elimu ili kuwajenga na kuwabadilisha kitabia," amesema SSP Mwangamilo.

Naye Bw. Mathias Kasabuku, Katibu wa Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki (CMPD) Wilaya ya Kigamboni, amesema elimu inayotolewa kupitia vyama vya bodaboda imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vurugu na kuboresha uendeshaji wa huduma hiyo na kuongeza nidhamu na heshima kwa waendesha Bodaboda.

Bw. Kasabuku ameongeza kuwa, licha ya changamoto za gharama za mafunzo na uendeshaji, viongozi wa vyama wanaendelea kuweka mikakati ya kuwafikia madereva kuanzia ngazi za chini hadi za juu ili kuhakikisha elimu ya usalama barabarani inawafikia madereva wote wanaoendesha Bodaboda.

LATRA inaendelea kufanya juhudi za kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini ili kupunguza athari zitokanazo na uendeshaji hovyo wa vyombo vya moto kibiashara.

> **"Zamani bodaboda walikuwa wakisababisha ajali na kuanzisha vurugu, lakini sasa uelewa umeongezeka. Pia Jeshi la Polisi linaendelea kufanya operesheni dhidi ya wavunjaji wa Sheria, na wale wanaokamatwa hupelekwa katika madawati ya elimu ili kuwajenga na kuwabadilisha kitabia,"**
>
> *SSP Solomon Mwangamilo*

# HUDUMA ZA USAFIRI WA WANAFUNZI ZAIMARISHWA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kuimarisha udhibiti wa huduma za usafiri wa mabasi ya mijini (daladala) kwa wanafunzi, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuhakikisha wanapata huduma salama, nafuu na ya uhakika wanapokwenda na kurudi kutoka shuleni.

Hayo yamebainishwa na Bw. Denis Daudi, Afisa Leseni na Usajili LATRA Machi 24, 2026 jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa Mamlaka imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa wadau wa usafirishaji ili kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kuwasafirisha wanafunzi kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa na Mamlaka.

“Tumekuwa tukitoa elimu kwa wadau wa usafirishaji ambao wanatoa huduma hii ya usafirishaji ili wafahamu umuhimu wa kuwasafirisha wanafunzi kwa wakati kutoka katika vituo wanavyopandia hadi kufika shuleni na kuwataarifu majina ya kila kituo ili wale wasiofahamu wajue ni kituo gani wanapaswa kushuka,” amesema Bw. Daudi.

Vilevile amesema, LATRA imeimarisha ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya daladala jijini Dar es salaam, mikoa mingine Tanzania Bara na kwenye magari yanayotoa huduma ya kubeba wanafunzi, ili kuhakikisha yanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za leseni za usafirishaji.

Amefafanua kuwa, nauli elekezi kwa mwanafunzi ni shilingi 200, kiwango ambacho kimewekwa na Mamlaka ili kumuwezesha kila mzazi kumudu gharama za usafiri huo na endapo atabainika mtoa huduma yeyote anatoza zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa, Mamlaka haitosita

*Inaendelea Uk 19 >>>*



*Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya msingi na sekondari jijini Dar es Salaam wakiingia kwenye usafiri unaomilikiwa na kampuni ya MOFAT inayotoa huduma maalum ya kubeba wanafunzi jijini Dar es Salaam kupitia awamu ya pili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Machi 10, 2026*

# HUDUMA ZA USAFIRI WA WANAFUNZI ZAIMARISHWA

<<< *Inatoka Uk 18*

kuchukua hatua dhidi yake kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Naye Bw. Joshua Changa, dereva wa daladala, amesema kuwa wanaendelea kuzingatia nauli elekezi ya shilingi 200 kama ilivyoelekezwa na LATRA, licha ya changamoto za uendeshaji wa huduma hiyo, na amewasihi makondakta wa daladala kutowakataa wanafunzi kwa kuwa ni sehemu ya abiria wanaopaswa kuhudumiwa kikamilifu na kuwapa kipaumbele wanapofika vituoni ili waweze kuwahi vipindi vyao shuleni.

Kwa upande wake Bw. Jackson Chavala kondakta wa daladala, amesema kuwa wanaendelea kujitahidi kutekeleza maelekezo na taratibu zilizowekwa na kutoa huduma bora kwa wanafunzi bila kikwazo na katika nyakati za asubuhi wanafunzi wasiopungua tano hadi kumi wamekuwa wakipakiwa katika kila daladala ili kuwawezesha kufika shuleni kwa wakati.

Bw. Joseph Kabogo ni mzazi wa mwanafunzi anayetumia huduma ya usafiri wa daladala amewashauri wazazi kuwapeleka watoto wao katika shule zilizo karibu na makazi yao ili kupunguza changamoto za kuchelewa kufika shuleni kutokana na changamoto za usafiri.

Juhudi za LATRA zinaendelea kulenga kuhakikisha huduma ya usafiri wa wanafunzi katika jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine inaboreshwa na kuendana na viwango vinavyotakiwa, ili kuwezesha wanafunzi kufika shuleni kwa wakati na kwa usalama.



*Wanafunzi wa Shule ya msingi wakiwa kwenye usafiri inaomilikiwa na kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) inayotoa huduma maalum ya kubeba wanafunzi jijini Dar es Salaam kupitia awamu ya kwanza ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Machi 18, 2026*

# LATRA YAWAJENGEA UWEZO KUSIMAMIA VTS




*Bw. Japhet Kabelege, Afisa Udhibiti Ubora – LATRA akiwapatia mafunzo ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) Maafisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kutoka Mkoa wa Lindi na Njombe walipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari kilichopo Ofisi za LATRA Mikocheni Dar es Salaam Februari 24, 2026.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kuwajengea uwezo maafisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) hatua inayolenga kuongeza usalama wa vyombo vya moto vinavyodhibitiwa nchini.

Hayo yamebainishwa na Bw. Mbwana Ndaro, Afisa Mfawidhi Kituo cha VTS wakati wa ziara ya mafunzo ya Maafisa hao kutoka mikoa ya Lindi na Njombe walipotembelea Kituo cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) cha LATRA kilichopo Mikocheni jijini Dar es Salaam Februari 24, 2026.

Bw. Ndaro, amesema kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha udhibiti wa usalama barabarani kupitia matumizi ya teknolojia, hususan katika kudhibiti mienendo isiyofaa ya madereva wa vyombo vya moto vinavyodhibitiwa na LATRA. Ameongeza kuwa, Mamlaka inaendelea kushirikiana kwa karibu na maafisa hao ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya usafiri ardhini.

"Mafunzo haya tuliyoyatoa kwa maafisa wa Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani yamewajengea uwezo mkubwa ambao utawezesha kufuatilia kwa ufanisi magari na mienendo ya madereva wanaodhibitiwa wanapotekeleza majukumu yao ya kuhakikisha usalama barabarani," amesema Bw. Ndaro.

Ameongeza kuwa, mfumo huo unawezesha LATRA kuchukua hatua stahiki pale panapobainika ukiukwaji wa Sheria au Kanuni za usalama barabarani, jambo linalochangia kuimarisha nidhamu kwa madereva na kulinda maisha ya abiria

*Inaendelea Uk 21 >>>*

## LATRA YAWAJENGEA UWEZO KUSIMAMIA VTS

<<< *Inatoka Uk 20*

pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

Kwa upande wake, SP James Makumu, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Lindi, ameishukuru LATRA kwa kutoa mafunzo hayo akisema yataongeza ufanisi katika usimamizi wa usalama barabarani, huku akiwataka wasafirishaji kuzingatia Sheria na kuhakikisha usalama wakati wa safari.

"Tunaishukuru LATRA kwa mafunzo haya, tumekuwa tukishirikiana katika nyanja mbalimbali za kazi zetu, na kupitia mafunzo haya tumeweza kupata uelewa na ujuzi zaidi kuhusu namna ya kusimamia Mfumo wa VTS. Hii itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu. Nitumie fursa hii kuwasihi wasafirishaji wote kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani ili kulinda usalama wa abiria na mali zake," amesema SP Makumu.

Ziara hiyo imelenga kuwapatia maafisa hao mafunzo ya kina kuhusu namna Mfumo wa VTS unavyofanya kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa usalama barabarani nchini.

## ABIRIA KUNUFAIKA NA TIKETI ZA MTANDAO ZENYE TAARIFA ZA BIMA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeendelea kuimarisha ushirikiano wake na wadau wa sekta ya usafiri ardhini, kwa lengo la kuongeza uelewa wa masuala ya bima na kuhakikisha taarifa za bima zinapatikana kupitia Mfumo wa tiketi mtandao ili kulinda haki za abiria na kuwawezesha abiria kupata fidia pindi wanapopata majanga au changamoto wanapokuwa safarini.

Akizungumza katika kikao kilichohusisha wadau wa sekta ya usafiri Ardhini kilichofanyika Februari 17, 2026 Ukumbi wa Mikutano ofisi za LATRA, Dar es Salaam, Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, amesema ni muhimu kwa kila tiketi ya safari anayopatiwa abiria kuwa na taarifa za kampuni ya bima na maboresho yanayotarajiwa kutekelezwa katika mfumo wa tiketi za mtandao yanalenga kuhakikisha taarifa hizo zinakuwepo na zinaonekana wazi kwa abiria ili waweze kuzitambua kwa urahisi.

Ameongeza kuwa, mara kadhaa LATRA imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa huduma za usafiri ardhini yanayohusu masuala ya bima na kutokana na ushirikiano mzuri uliokuwepo na TIRA, malalamiko hayo yamekuwa yakishughulikiwa kwa taratibu zilizowekwa.

"Mamlaka imekuwa ikipokea malalamiko yanayohusu masuala ya bima kutoka kwa watumiaji wa huduma za usafiri ardhini, na kwa kushirikiana na TIRA tumekuwa tukiyatatua kwa pamoja. Ushirikiano huu ni endelevu na umeanza tangu hatua za awali za uundaji wa mfumo wa tiketi za mtandao. Maboresho tunayoyafanya yanalenga kumwezesha abiria kufahamu kama tiketi aliyokata ina taarifa za bima na ni kampuni ipi inahusika, ili aweze kupata fidia pindi atakapokumbwa na changamoto kama ajali akiwa safarini," amesema Bw. Pazzy.

*Inaendelea Uk 22* >>>

# ABIRIA KUNUFAIKA NA TIKETI ZA MTANDAO ZENYE TAARIFA ZA BIMA

<<< *Inatoka Uk 22*

Kwa upande wake, Bw. Christopher Geofrey Mapunda, Mkurugenzi wa Leseni na Msimamizi wa Bima Mtawanyo wa TIRA, amesema kikao hicho kimeandaliwa mahsusi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wadau wa sekta ya usafirishaji kuhusu umuhimu wa kuweka jina la kampuni ya bima kwenye tiketi mtandao anayopatiwa abiria.

"Serikali imelenga kuhakikisha tiketi zote za usafiri zinakuwa na taarifa za kampuni ya bima ili, ikitokea ajali au dharura, mwananchi aweze kufahamu hatua za kuchukua na wapi pakuanzia katika kudai haki yake, TIRA itaendelea kusimamia utekelezaji wa miongozo ya bima ili kuhakikisha kampuni za bima zinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Serikali, huku ikiendelea kuboresha mifumo ya upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko kutoka kwa wananchi," amesema Bw. Mapunda.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa usafirishaji, Bw. Joseph Didas, Mkurugenzi wa Kampuni ya Mabasi ya Esther Luxury Coach, amesema kikao hicho kimekuwa na manufaa makubwa kwao kupitia elimu waliyoipata na ametoa pongezi kwa maboresho yanayoenda kufanyika kwa kuwa yatasaidia kuongeza imani kwa wasafirishaji na kulinda haki za abiria.

LATRA imeendelea kushirikisha wadau wa sekta ya usafiri ardhini nchini katika kila hatua ya maboresho ya huduma zinazoenda kutekelezwa kwa lengo la kuhakikisha huduma za usafiri zinakuwa salama, bora na zenye kuzingatia haki za watumiaji.




***Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) akiongoza kikao kilichohusisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) na wadau wa sekta ya usafiri ardhini kuhusu umuhimu wa kuweka taarifa za kampuni ya bima kwenye tiketi mtandao. Kikao hicho kimefanyika Februari 17, 2026 Ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA, Dar es Salaam.***

# LATRA YAWANOA WATUMISHI WA TRC




*Wafanyakazi Mahususi wa Reli (Safety Critical Workers) wanaohusika na uendeshaji wa treni za Reli ya Kisasa (SGR) za Shirika la Reli Tanzania (TRC) wakipatiwa elimu ya usalama kwa madereva wa treni kuhusu mwenendo sahihi wanapokuwa kazini ili kuzuia hatari na ajali zinazoweza kusababishwa na uzembe. Mafunzo hayo yamefanyika Februari 16, 2026 Stesheni ya John Magufuli, Dar es Salaam.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa semina ya kuwajengea uwezo Wafanyakazi muhimu wa usalama katika undeshaji wa reli (Safety Critical Workers) ikiwemo madereva na waongoza treni wa Treni ya Kisasa (SGR) kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa uweledi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi utakaosaidia kupunguza ajali zitokanazo na makosa ya kibinadamu.

Hayo yamesemwa na Mha. Moses Nyoni, Afisa Mkaguzi wa Reli Mwandamizi LATRA aliyemuwakilisha Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli LATRA katika semina iliyofanyika Februari 16, 2026 Stesheni ya John Magufuli, Dar es Salaam.

"Semina hii imelenga kuwakumbusha wataalamu wetu majukumu yao pamoja na namna bora ya mwenendo wao wawapo kazini, hii itasaidia kupunguza makosa ya kibinadamu yanayoweza kusababisha ajali, hivyo madereva na waongoza treni wakiwa kama watu wa mbele katika mfumo wa treni kufanya kazi, tunao wajibu wa kuwaelimisha na kuwakumbusha masuala ya usalama," amesema Mha. Nyoni.

Vilevile amesema, "Mafunzo haya yatasaidia sana katika kuondoa makosa ya kibinadamu miongoni mwenu kwani makosa hayo husababisha hasara nyingi na kubwa kwa taifa ikiwemo ajali za treni ambazo huharibu miundombinu ya reli na treni yenyewe lakini pia kuepuka kupata harasa za mali na hata kupoteza maisha kwa abiria wanaotumia vyombo hivyo,"

Akizunguza baada ya mafunzo haya Mha. John Ngaraguza, Mkufunzi wa Masuala ya Reli amesema kuwa, semina hiyo imejikita katika kuamsha morali ya kazi, na kupunguza viashiria vinavyoweza kuchochea makosa ya kibinadamu kama

*Inaendelea Uk 24* >>>

# LATRA YAWANOA WATUMISHI WA TRC

<<< Inatoka Uk 22

vile msongo wa mawazo, uchovu na ufanyaji kazi kimazoea.

"Semina hii imewalenga Madereva wa Treni, waongoza Treni (Train controllers) wanaohusika na Treni ya Kisasa (SGR) ambapo pamoja na yote wamejengewa uwezo wa kuutumia kiufasaha mfumo wa uongozaji treni uliopo kwa sasa," amesema Ngaraguza.

Kwa upande wao, washiriki wa mafunzo hayo wameishukuru LATRA kwa kuwapatia mafunzo hayo kwani yamewapatia mwanga na kuwafanya wawe tayari zaidi kuitumikia sekta ya reli na taifa kwa jumla ili kuleta maendeleo ya pamoja katika sekta ya usafiri wa reli nchini.

> **"Mafunzo haya yatasaidia sana katika kuondoa makosa ya kibinadamu miongoni mwenu kwani makosa hayo husababisha hasara nyingi na kubwa kwa taifa ikiwemo ajali za treni ambazo huharibu miundombinu ya reli na treni yenyewe lakini pia kuepuka kupata harasa za mali na hata kupoteza maisha kwa abiria wanaotumia vyombo hivyo,"**
>
> *Mha. Moses Nyoni*

---

# MAWAKALA WA LATRA MOROGORO WANOLEWA KUHUSU RUSHWA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Morogoro imetoa elimu ya rushwa kwa maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (Pikipiki na Bajaji) wanaotoa leseni za vyombo vya usafiri wa kukodi kwa niaba ya Mamlaka ikiwa ni sehemu ya jitihada za makusudi za LATRA katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa, pamoja na kuimarisha uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za usafiri ardhini.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo Februari 11, 2026 mkoani Morogoro Bw. Andrew Mlacha, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Morogoro, amesema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha huduma za usafiri zinatolewa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo, huku wananchi wakipata huduma bora bila usumbufu wala mianya ya vitendo visivyo halali.

Aidha, Bw. Mlacha amesisitiza umuhimu wa kutumia mifumo rasmi ya malipo, akieleza kuwa waombaji wa leseni wanapaswa kufanya malipo kupitia namba maalumu ya malipo (Control Number) ili kuepuka malipo ya ziada au yasiyo rasmi yanayokiuka viwango vilivyowekwa na Mamlaka.

"Serikali imeweka mifumo rasmi ya malipo kwa kutumia namba maalumu ya malipo (Control Number), hivyo hakuna wakala anayeruhusiwa kupokea

Inaendelea Uk 25 >>>

# MAWAKALA WA LATRA MOROGORO WANOLEWA KUHUSU RUSHWA

<<< *Inatoka Uk 24*

fedha taslimu mkononi kinyume na utaratibu uliowekwa. Endapo atabainika yeyote kukiuka taratibu hizo, hatua kali zitachukuliwa mara moja ikiwemo kufutiwa leseni ya uwakala," amesema Bw. Mlacha.

Vilevile, mawakala hao wamepatiwa elimu kuhusu umuhimu wa kuvaa sare maalumu pamoja na vitambulisho vya kazi wanapotekeleza majukumu yao, ili waweze kutambulika kwa urahisi na kuepusha migogoro isiyo ya lazima baina yao na wananchi.

Aidha, wamehimizwa kutumia lugha za staha katika utekelezaji wa majukumu yao, huku wakikumbushwa kuwa kauli njema ni chachu ya kuboresha huduma kwa wananchi, wakati lugha isiyo na staha huathiri utoaji wa huduma na kuchochea migogoro kati ya Mamlaka na watoa huduma.

Kwa upande wao, maafisa usafirishaji walioshiriki mafunzo hayo wameipongeza LATRA pamoja na Serikali kwa kuwawezesha kupata elimu hiyo muhimu, wakieleza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kuboresha utendaji kazi wao na kutatua changamoto zilizokuwepo awali katika utoaji wa leseni.

Serikali kwa kushirikiana na LATRA inaonesha dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha uwajibikaji, nidhamu na ufanisi katika sekta ya usafiri ardhini, hususan huduma za vyombo vya usafiri wa kukodi ambazo zinaendelea kukua kwa kasi mkoani Morogoro na nchini kwa jumla.



*Bw. Andrew Mlacha, Afisa Mfawidhi LATRA Mkoa wa Morogoro akitoa elimu ya rushwa kwa maafisa usafirishaji wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (Pikipiki na Bajaji) wanaotoa leseni za vyombo vya usafiri wa kukodi kwa niaba ya Mamlaka. Elimu hiyo imetolewa Februari 11, 2026 Mkoani Morogoro.*

# MHE: MUTASINGWA ELIMU YA MIFUMO YA LATRA NI MUHIMU KWA WANANCHI




Mhe. Mha. Johnston Mutasingwa (Mb) Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu (PIC) ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuendelea kutoa elimu kuhusu mifumo ya Teknojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa na Mamlaka katika shughuli zake za kiudhibiti ili kuongeza uwazi, ufanisi na ushiriki wa wananchi katika sekta ya usafiri ardhini.

Mhe. Mutasingwa amebainisha hayo Februari 16, 2026 wakati wajumbe wa Kamati ya PIC walipotembelea ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya ziara maalum ya kujifunza jinsi LATRA inavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

"Tunawapongeza LATRA kwa juhudi kubwa za kurahisisha upatikanaji wa taarifa za usafiri ardhini kwa wananchi. Hata hivyo, tunasisitiza muendelee kutoa elimu kwa kuhusu mifumo mnayoitumia ili wananchi waweze kufahamu LATRA inafanya nini na elimu hii ikiwafikia wananchi ambao ndio watumiaji wa huduma za usafiri ardhini maswali mengi ambayo wamekuwa wakijiuliza yatapungua na itaongeza ufanisi katika utendaji kazi wenu," amesema Mhe. Mtasigwa.

Kwa upande wake, CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA, amesema kuwa Mamlaka ina mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayorahisishia utoaji wa huduma za usafiri ardhini ikiwemo Mfumo wa Safari Tiketi, unaorahisisha upatikanaji wa tiketi za mabasi ya masafa marefu na usafiri wa Treni ya Kisasa (SGR), Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS), unaomuwezesha abiria kufuatilia mwenendo wa safari na kutambua mahali basi lilipo na Mfumo Tumizi wa LATRA APP, unaomuwezesha abiria kuhakiki tiketi za safari, kupata taarifa za viwango vya nauli za mabasi ya mijini (daladala) na mabasi ya masafa marefu, na wasafirishaji wanaweza kuhakiki uhai wa leseni zao.

Aidha, CPA, Dkt. Suluo ameeleza kuwa LATRA pia inatumia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli (RRIMS) ambao ni mfumo mama wa Mamlaka unaosaidia katika usimamizi na udhibiti wa shughuli za usafiri ardhini kwa jumla.

*Inaendelea Uk 27* >>>

## MHE: MUTASINGWA ELIMU YA MIFUMO YA LATRA NI MUHIMU KWA WANANCHI

*<<< Inatoka Uk 27*

Naye Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa LATRA, ameishukuru Kamati ya PIC kwa ziara hiyo na ameahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa, ikiwemo kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na LATRA katika shughuli zake za udhibiti.

Elimu ya mifumo ya LATRA ni nyenzo muhimu katika kuimarisha udhibiti wa sekta ya usafiri ardhini na kufanikisha lengo la Serikali la kuwa na huduma za usafiri zilizo salama, bora na endelevu.

## CPA, DKT. SULUO AWASIHI WATUMISHI WA LATRA KUFANYA KAZI KWA BIDII NA KUJITUMA

CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewasihi watumishi wa LATRA kufanya kazi kwa moyo, bidii na kujituma huku wakizingatia Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS) ISO 9001 ili kuacha tabasamu kwa wateja.

CPA, Dkt. Suluo amebainisha hayo Januari 16, 2026 katika Kikao cha Saba cha Baraza la Wafanyakazi la LATRA linachofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Magadu ,Mkoani Morogoro

“Tumepata ithibati ya Kimataifa ya kutoa huduma kwa viwango vya kimataifa hivyo tuendelee kutoa huduma bora kwa wateja tunaowahudumia. Tuendelee kushikamana tukitambua kuwa tupo kwenye nafasi zetu kumsaidia Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo ni jukumu la kila mmoja wetu kutafakari tunachokifanya ili kuleta nyuso za tabasamu kwa wananchi,” amesema CPA, Dkt. Suluo.

Vilevile amesema kuwa, anajivunia kuwa na watumishi wanaofanya kazi kwa juhudi na mafanikio ya LATRA yaliyopatikana ni matokeo ya utendaji mzuri wa watumishi hao.

Naye Bw. Mussa Mwakalinga, mwakilishi kutoka Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania – COTWU (T) amempongeza CPA, Dkt. Suluo, mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi LATRA kwa kuboresha Baraza hilo na kuendesha vikao hivyo kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kikao hicho kinafanyika kwa siku mbili Januari 16 na 17, 2026 ambapo wajumbe wa Baraza hilo wamepatiwa mafunzo ya siku moja kuhusu Afya ya Moyo, Sheria ya Mirathi, Haki za Watoto pamoja na Sheria ya Ndoa.

Kwa nyakati tofauti, wajumbe wa Baraza hilo wamepongeza mada zilizowasilishwa na wataalamu na wamesema elimu waliyopatiwa inaendana na mahitaji halisi yaliyopo.

Baraza la Wafanyakazi la LATRA linaendesha vikao vyake mara moja kwa mwaka na linajumuisha Wajumbe wa Menejimenti, Wawakilishi wa Watumishi wa Idara na Vitengo, Maofisa Wafawidhi wa Mikoa yote pamoja na Uongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania – COTWU (T) - Tawi la LATRA

# MAGOMBANA: KANUNI HIZI NI MUHIMU KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRISHAJI




*Bw. Andrew Magombana, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri kwa njia ya Barabara Wizara ya Uchukuzi, akifungua rasmi Mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu mapendekezo ya Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2026, Ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Utalii Dar es Salaam Januari 8, 2026.*

Bw. Andrew Magombana, Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa njia ya Barabara Wizara ya Uchukuzi amesema rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026 ni nyenzo muhimu ya kuimarisha sekta ya usafirishaji nchini,

Bw. Magombana amesema hayo Januari 8, 2026 katika mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026, ukumbi wa Mikutano Chuo cha Utalii Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Bw. Magombana ameeleza kuwa zipo changamoto mbalimbali katika usimamizi wa vyombo vya moto kibiashara zinazoongeza uhitaji wa kuwa na Kanuni hizo muhimu zinazolenga kuwasimamia watoa huduma za usafiri na madereva katika usimamizi wa madhara yanayotokana na uchovu wakati wakiendesha vyombo ambavyo vinadhibitiwa na Mamlaka.

"Changamoto ambazo zimeonekana ni kutokuwepo kwa Kanuni mahsusi za kushughulikia na kufanya udhibiti katika usimamizi wa uchovu wa madereva wa vyombo vya usafiri kwa njia ya barabara, kuwepo kwa ongezeko la ajali mbalimbali zinazosababishwa na uchovu wa madereva hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imeruhusu mabasi ya abiria kufanya kazi saa 24 na kukosekana kwa nyenzo ya kulinda afya za madereva wa usafiri ardhini ili kuhakikisha wanapata muda wa kutosha kupumzika," amesema Bw. Magombana.

Vilevile amesema, wamiliki wa vyombo vya moto kibiashara wanatakiwa kuandaa mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu kwa lengo la kuimarisha sekta ya usafirishaji.

*Inaendelea Uk 29* >>>

# MAGOMBANA: KANUNI HIZI NI MUHIMU KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA USAFIRISHAJI

*<<< Inatoka Uk 28*

"Rasimu ya Kanuni hizi zimetoa wajibu kwa madereva na kwa wamiliki wa vyombo katika usimamizi wa madhara ya uchovu ambapo wamiliki wanatakiwa kuandaa mpango wa usimamizi wa madhara ya uchovu na Matarajio ya Serikali ni kwamba, endapo kila mmoja atatimiza kikamilifu wajibu wake kama ilivyoainishwa katika Rasimu ya Kanuni hizi, ubora na usalama wa usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya barabara utaongezeka," ameeleza Bw. Magombana.

Kwa upande wake CPA, Dkt. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amesema kuwa, uchovu wa madereva ni miongoni mwa sababu kubwa zinazosababisha ajali za barabarani ambazo zinagharimu maisha ya watu na mali zao.

"Dereva anapochoka na kuendelea kuendesha gari, hatari ya ajali huwa kubwa na ikitokea tunapoteza uhai wa watu, wengine wanapata ulemavu na taifa linaingia gharama kubwa za matibabu na kupoteza nguvu kazi. Kanuni hizi zinalenga kuweka mifumo madhubuti ya kudhibiti muda wa kazi na mapumziko ya madereva, usimamizi wa ratiba za safari, pamoja na wajibu wa waajiri na wamiliki wa vyombo vya usafiri katika kuhakikisha usalama unazingatiwa," amesema CPA, Dkt. Suluo.

Vilevile CPA, Dkt. Suluo amesema, Serikali imeona umuhimu wa kuchukua hatua mapema ili kuzuia madhara makubwa yanayotokana na uchovu wa madreva, hususan katika usafiri wa masafa marefu na usafirishaji wa mizigo na kulinda mitaji ya wawekezaji, kulinda afya na usalama wa madereva wao na hasa kulinda uhai wa wananchi .

Rasimu za Kanuni za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2026, zimeandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na LATRA na zinapatikana kwenye tovuti ya LATRA www.latra.go.tz ambapo wadau wanaweza kuwasilisha maoni yao kwa maandishi kupitia baruapepe group.maoni@latra.go.tz hadi tarehe 22 Januari 2026 ikiwa ni siku 14 baada ya mkutano huo.

**"kuwepo kwa ongezeko la ajali mbalimbali zinazosababishwa na uchovu wa madereva hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali imeruhusu mabasi ya abiria kufanya kazi saa 24 na kukosekana kwa nyenzo ya kulinda afya za madereva wa usafiri ardhini"**

*Bw. Andrew Magombana*






<< *Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Reli wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), akiongoza mafunzo kwa Wafanyakazi Mahususi wa Reli (Safety Critical Workers) wanaohusika na uendeshaji wa treni za Reli ya Kisasa (SGR) za Shirika la Reli Tanzania (TRC) yaliyofanyika Stesheni ya Jakaya Kikwete Morogoro Februari 19, 2026*

*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) wakiwa kwenye mafunzo Januari 16, 2026, ukumbi wa Mikutano Magadu, Mkoani Morogoro ambapo walijifunza kuhusu Afya ya Moyo, Sheria ya Mirathi, Haki za Watoto pamoja na Sheria ya Ndoa.* >>





<< *Prof. David Mfinanga, Mwenyekiti wa Kamati ya kuandaa andiko la mapendekezo ya namna bora ya kusimamia huduma bora za usafiri wa Pikipiki akiongoza kikaokazi kati ya kamati hiyo na Shirikisho la Waendesha Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam na Taifa, Machi 23, 2026 ofisi za LATRA Dar es Salaam.*



LATRA

IMETHIBITISHWA ISO 9001

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), likiongozwa na Bodi ya Wahariri;**

Mwenyekiti: **CPA DKT. HABIBU SULUO** | Mhariri Mkuu: **SAMUEL KEENJA** | Wahariri Wasaidizi: **SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE** | Waandishi: **MAMBWANA JUMBE, MARYAM NINA** na **NANCY AMANI** | Wasanifu Jarida: **DEUSDEDITY MASEMBA** na **IBRAHIM SAID**

**©2026**